**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**


*Simu+255262963313/2963314*
*Nukushi: +255 26 296 3316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali Mtumba,*
*S. L. P 2908,*
***40477 DODOMA***


***Kumb.Na JA.173/176/01A/146*** ***06 Novemba, 2025***

# TANGAZO

## NAFASI YA UDALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA

**Kanuni ya 6 ya Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka, (Tangazo la Serikali Na. 172 la 2023)**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakaribisha maombi ya Udalali wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa **Mikoa ya Iringa, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mtwara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora.** Waombaji wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo.

**Sifa.**

1. Awe Raia na mkazi wa Tanzania mwenye akili timamu ambaye ametimiza umri wa utu uzima;
2. Awe ni mkurugenzi wa kampuni iliyosajiliwa Tanzania au mshirika wa Taasisi iliyosajiliwa;
3. Awe Dalali halali wa Mahakama (*Court Brokers*);
4. Awe na Leseni hai ya Udalali *(Auctioneer's General Licence*);
5. Awe na Leseni hai ya Biashara katika eneo husika analotaka kufanyia kazi;
6. Awe na Cheti kuhusu kazi za udalali kilichotolewa na Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto au chuo chochote kinachotambulika na serikali;
7. Awe na elimu ya kidato cha nne au inayolingana nayo na anafahamu vyema lugha ya Kiswahili na Kiingereza;
8. Awe mtu safi, raia mwema asiye na kumbukumbu zozote za makosa ya jinai au utapeli wa mali za watu anazonadi;
9. Awe na Mkataba hai wa pango la Ofisi yenye Bima kwa ajili ya kufanyia kazi na kutunzia Kumbukumbu;
10. Awe na Ghala lenye Bima kwa ajili ya kuhifadhi mali; na
11. Anayeomba nafasi hiyo ya Udalali asiwe: -
    (a) amewahi kubatilishiwa cheti chake cha kuwa Dalali chini ya Kanuni hizi au sheria nyingine zozote;

    (b) ni Jaji, Hakimu au Mwenyekiti wa Baraza au mtu aliyeajiriwa kwa nafasi yoyote kama mtendaji au afisa wa Baraza;

(c) ni wakili anayefanya shughuli za kiwakili;

(d) ni mbunge au diwani;

(e) ni mtumishi wa umma na ambaye majukumu yake yana mgongano wa maslahi na kazi za udalali; au

Maombi yawasilishwe kwa kujaza Fomu Na.3 ya **Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka (Tangazo la Serikali Na. 172 la 2023).**

Aidha, maombi yaambatishwe na risiti ya malipo ya ada ya maombi ya kiasi cha Shilingi **250,000**/=. Namba ya malipo (Control Number) itatolewa katika Ofisi ya Baraza lililo karibu.

Maombi yote yamfikie Katibu wa Kamati kabla ama ifikapo tarehe 28 Novemba, 2025 kupitia anuani kama inavyoonekana hapa chini.

**Katibu,**
Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi,
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
S.L.P. 2908,
**DODOMA.**